TANGAZO LA SERIKALI Na. 60 la tarehe. 10/2/2023

SHERIAYA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA,
(SURA YA 306)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 165)*

KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA KUHUSU USAJILI WA LAINI ZA SIMU, 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MAHITAJI YA USAJILI WA LAINI ZA SIMU

4. Wajibu wa kusajili laini ya simu.
5. Wajibu wa mtoa huduma.
6. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mtu binafsi.
7. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa kampuni.
8. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa wafanyakazi wa kampuni.
9. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa taasisi.
10. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mtoto.
11. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mgeni wa muda mfupi.
12. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mgeni.
13. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mkimbizi.

14. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mdiplomasia.
15. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa taasisi za kidiplomasia.
16. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu itakayotumika kwenye kifaa cha kielektroniki au mashine.
17. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mteja mwenye kasoro kwenye alama za vidole au asiye na vidole.
18. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa baadhi ya watu.
19. Utaratibu wa kusajili upya Laini ya simu.
20. Zuio la kutumia Kitambulisho cha Taifa.
21. Haki ya kusajili Laini ya simu bila kuhakiki kibayometriki.
22. Taarifa za ziada.

SEHEMU YA TATU
KUHUISHA NA KUSITISHA MATUMIZI YA LAINI ZA SIMU

23. Laini za simu hai.
24. kuhuisha PIN ya kufungua na kufunga laini ya simu.
25. Kusitisha matumizi ya Laini ya simu.
26. Utaratibu kuhusu bakaa ya fedha.
27. Uwasilishaji wa taarifa za laini ya simu zilizositishwa matumizi kwa Mamlaka.

SEHEMU YA NNE
UTUMIAJI WA MAWAKALA KATIKA USAJILI WA LAINI ZA SIMU

28. Utumiaji wa mawakala kwenye usajili wa laini ya simu.
29. Vigezo vya uwakala.
30. Mtoa huduma kuwasilisha taarifa za kila mwezi.

SEHEMU YA TANO
UBADILISHAJI WA TAARIFA AU UMILIKI

31. Ubadilishaji wa taarifa na umiliki.
32. Jukumu la kutoa taarifa ya upotevu wa laini ya simu.
33. Ubadilishaji wa laini ya simu.
34. Kuhamisha taarifa kwenye laini ya simu.

MASHARTI YA JUMLA

35. Ukaguzi wa wakala.
36. Vitendo vya udanganyifu.
37. Idadi ya laini za simu zinazoweza kumilikiwa.
38. Uhakiki wa laini za simu zilizosajiliwa.
39. Kosa kwa matumizi mabaya ya taarifa.
40. Adhabu ya jumla.
41. Kufutwa.

SHERIAYA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA,
(SURA YA 306)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 165)*

KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA KUHUSU USAJILI WA LAINI ZA SIMU, 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023.

Matumizi

2.-(1) Kanuni hizi zitatumika kwa watumiaji wote wa laini za simu katika Jamhuri ya Muungano.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kanuni ndogo ya (1), Kanuni hizi hazitatumika kwa watumiaji wa laini za simu zilizotolewa au kusajiliwa nje ya nchi ambazo zinafanya kazi nchini kupitia mitandao ya simu ya watoa huduma wa ndani.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"aina za usajili wa laini za simu kibayometriki" inajumuisha kampuni, mdiplomasia, mtu binafsi, taasisi, mgeni, mtoto, mkimbizi, mgeni wa muda mfupi au aina nyingine yoyote kama itakavyoamuliwa na Mamlaka mara kwa mara;

"Idara ya Uhamiaji" maana yake ni Idara ya Uhamiaji Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Uhamiaji;

"kuhuisha matumizi ya laini ya simu" maana yake ni

kuifanya laini ya simu iweze kufanya kazi katika mtandao wa simu;

"kundi la laini za simu" maana yake ni laini za simu zaidi ya moja zilizosajiliwa kwa pamoja kwa ajili ya mawasiliano ya kielektroniki na kwa kutumia kitambulisho cha taifa na alama za vidole za mwakilishi mmoja pasipo laini za ziada;

"laini ya simu" maana yake ni moduli ya utambulisho wa mteja ambayo ni kadi inayojitegemea iliyowashwa kielektroniki iliyoundwa kwa ajili ya matumizi pamoja na simu ya mkononi ili kumwezesha mtumiaji kutuma na kupokea mawasiliano ya kielektroniki;

"laini ya simu hai" maana yake ni laini ya simu inayofanya kazi katika mtandao wa simu;

"kifaa cha mawasiliano ya simu" maana yake ni kifaa kinachotumika kwa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi ikijumuisha vifaa vinavyotumia huduma za mtandao katika mitandao ya simu;

Sura ya 172

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliyoanzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania;

"mawasiliano ya mashine kwa mashine" maana yake ni mawasiliano ya moja kwa moja kati ya vifaa ili kubadilishana taarifa na kufanya vitendo bila uingiliaji wa mwanadamu;

Sura ya 356

"mdiplomasia" maana yake ni mtu ambaye yuko kwenye kazi ya kidiplomasia katika Jamhuri ya Muungano kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kinga na Haki za Kidiplomasia na Kibalozi;

"mgeni" maana yake ni mtu asiye raia wa Tanzania au mdiplomasia anayekaa nchini kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita;

"mgeni wa muda mfupi" maana yake ni mtu asiye raia ambaye si mdiplomasia na anatarajia kukaa katika Jamhuri ya Muungano kwa muda usiozidi miezi minne;

"mkataba wa huduma" maana yake ni makubaliano yaliyoingiwa kati ya mtoa huduma na mteja kwa ajili ya utoaji wa huduma zilizotolewa leseni kwa

wateja;

Sura ya 37

mkimbizi" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Wakimbizi;

"mlaji" maana yake ni mtu yeyote anayetumia bidhaa au huduma za mawasiliano ya kielektroniki au posta;

"mlezi" maana yake ni mtu ambaye ana wajibu, udhibiti au usimamizi kwa mtoto au mtu aliyeteuliwa kwa hati, wosia au amri ya mahakama aliyepewa jukumu la kutunza na kusimamia mali na haki za mtoto;

"mteja" maana yake ni mtu yeyote anayepata au aliyeomba kupata huduma ya aina yoyote kutoka kwa mtu anayefanya kazi kwa mujibu wa Kanuni hizi na inajumuisha wateja wa kampuni za simu;

"mtoa huduma" maana yake ni mtu aliyepewa leseni na Mamlaka ya kutoa na kuwezesha utoaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroniki;

"mtoto" maana yake ni mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na minane na zaidi ya miaka kumi na miwili;

Sura ya 306

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta;

"taasisi" maana yake ni serikali au taasisi isiyo ya kiserikali inayofanya kazi ndani ya Jamhuri ya Muungano;

"taasisi ya kidiplomasia" maana yake ni taasisi ya kimataifa yenye vibali vya kidiplomasia kwa Jamhuri ya Muungano;

"usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa mgeni" maana yake ni aina ya usajili wa laini za simu kibayometriki itakayotumika kwa ajili ya matumizi ya mgeni pekee;

"usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa mgeni wa muda mfupi" maana yake ni aina ya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa ajili ya matumizi ya mgeni wa muda mfupi pekee; na

"usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kampuni" maana yake ni aina ya usajili wa laini ya simu kibayometriki itakayotumika kwa ajili ya matumizi ya kampuni pekee;

Sura ya 54

“usajili wa laini za simu kibayometriki kwa mtu binafsi” maana yake ni aina ya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa ajili ya matumizi ya mtu binafsi pekee;

“usajili wa laini ya simu kwa mdiplomasia” maana yake ni aina ya usajili wa laini ya simu kibayometriki itakayotumika kwa ajili ya matumizi ya mdiplomasia pekee;

"usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa mtoto" maana yake ni aina ya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa ajili ya matumizi ya mtoto pekee;

“usajili wa laini za simu kibayometriki kwa taasisi” maana yake ni aina ya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa ajili ya matumizi ya taasisi pekee;

“usajili wa laini za simu kwa taasisi za kidiplomasia” maana yake ni usajili wa laini za simu kibayometriki itakayotumika kwa ajili ya matumizi ya taasisi za kidiplomasia pekee;

“nambari tambulishi” maana yake ni msimbo wa kipekee unaotumika kutambua simu binafsi katika mtandao wa Mifumo ya Mawasiliano ya Simu ya Kimataifa;

“PIN” maana yake ni nambari pekee inayotumika kufungua na kufunga laini ya simu;

“wakala” maana yake ni chombo au mtu anayesajili laini za simu kwa niaba ya mtoa huduma;

“wakala asiye na ofisi” maana yake ni wakala anayeruhusiwa kufanya kazi katika eneo maalum la kijiografia;

## SEHEMU YA PILI
## TARATIBU ZA USAJILI WA LAINI ZA SIMU

Wajibu wa kusajili laini ya simu

4.-(1) Mtu yeyote anayemiliki, anadhibiti au anakusudia kutumia laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu-

(a) atasajili kibayometriki laini ya simu

inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu kwa mtoa huduma husika au wakala aliyeidhinishwa kwa namna iliyoainishwa katika Kanuni hizi;

(b) atahakikisha PIN ya laini yake ya simu haijulikani na mtu mwingine yeyote; na

(c) atamtaarifu mtoa huduma wake kuhusu mabadiliko ya mtumiaji au matumizi ya kila laini ya simu anayoimiliki.

(2) Mtu yeyote ambaye anauza au kwa namna nyingine yoyote anatoa laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu kwa mteja yeyote -

(a) atasajili laini za simu za wateja kwa kutumia taratibu kama zilivyoainishwa katika kanuni hizi; na

(b) atatunza kumbukumbu za taarifa ya usajili wa laini za simu katika kanzidata kama zitakavyochukuliwa kielektroniki kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa au Idara ya Uhamiaji.

(3) Kila mtoa huduma atahakikisha kuwa-

(a) mfumo wake wa usajili umeunganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, unafanya kazi na unapatikana muda wote.

(b) mfumo wake wa usajili umeunganishwa na kanzidata kuu ya usajili wa laini za simu ya Mamlaka, unafanya kazi na unapatikana muda wote.

(c) taarifa za usajili wa laini ya simu zilizohakikiwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa au Idara ya Uhamiaji zinawasilishwa moja kwa moja kwenye kanzidata kuu ya usajili wa laini za simu ya Mamlaka wakati wa mchakato wa usajili; na

(d) ubadilishaji wa laini ya simu iliyoharibika unafanyika baada ya kuhakiki kibayometriki

usajili na umiliki wa awali wa mhusika.

(4) Mtu hatasajili laini yoyote ya simu kwa kutumia kitambulisho cha taifa cha mtu mwingine isipokuwa kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi.

Wajibu wa Mtoa huduma

5.-(1) Mtoa huduma ataweka utaratibu wa uthibitisho ili kuhakikisha kwamba laini za simu zinasajiliwa kwa ajili ya wateja waliokusudiwa.

(2) Baada ya kukamilisha usajili wa laini ya simu, mtoa huduma atatuma ujumbe mfupi wa maneno kwenye laini zote za simu za mteja ukionesha jina la wakala aliyefanya usajili, namba ya kitambulisho cha taifa cha wakala na orodha ya laini zote za simu zilizosajiliwa na mteja kwa watoa huduma wote.

(3) Baada ya ufutaji, ubadilishaji au uhuishaji wa usajili wa laini ya simu, mtoa huduma atatuma taarifa ya ujumbe mfupi wa maneno kwenye laini za simu za mteja zilizosajiliwa ukionesha jina la wakala aliyefanya mabadiliko, namba ya kitambulisho cha taifa ya wakala na orodha kamili ya laini za simu zilizosajiliwa na mteja kwa watoa huduma wote.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mtu binafsi

6. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mtu binafsi utakuwa kama ifuatavyo-

(a) mtu binafsi atawasilisha kwa mtoa huduma kitambulisho cha taifa au namba ya kitambulisho cha taifa;
(b) mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;
(c) mtoa huduma atatunza taarifa za mteja kama zilivyochukuliwa kielektroniki kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; na
(d) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa na jina la mtu binafsi kama linavyosomeka katika mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Utaratibu wa

7. Utaratibu wa kusajili laini za simu endapo

usajili wa laini ya simu kwa kampuni

mteja ni kampuni utafanyika chini ya usajili wa laini za simu kibayometriki kwa kampuni kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo:

(a) mwakilishi wa kampuni atawasilisha barua ya utambulisho, nakala ya cheti halali kilichothibitishwa chenye Namba ya Mlipa Kodi, leseni ya biashara na cheti cha usajili wa kampuni au cheti cha utekelezaji wa kazi husika;

(b) mwakilishi wa kampuni atawakilisha kitambulisho chake cha taifa au namba ya kitambulisho cha taifa kwa mtoa huduma;

(c) mtoa huduma atafanya usajili wa kundi la laini za simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za muwakishi wa kampuni mara moja kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;

(d) mtoa huduma atatunza taarifa za kampuni na za mwakilishi wa kampuni;

(e) laini za simu zilizosajiliwa zitakuwa kwa jina la kampuni; na

(f) kampuni itamtaarifu mtoa huduma kuhusu mabadiliko ya mwakilishi wa kampuni kwa ajili ya mtoa huduma kumsajili mwakilishi mpya kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa wafanyakazi wa kampuni

8. Utaratibu wa kusajili laini za simu kwa wafanyakazi wa kampuni, utafanyika chini ya usajili wa laini za simu kibayometriki kwa wafanyakazi wa kampuni kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo-

(a) kampuni itawasilisha barua ya utambulisho, nakala ya cheti halali kilichothibitishwa chenye Namba ya Mlipa Kodi, leseni ya biashara na cheti cha usajili au cheti cha utekelezaji wa kazi husika;

(b) mfanyakazi wa kampuni ambaye anastahili kutumia laini ya simu atatakiwa kuwasilisha kwa mtoa huduma kitambulisho chake cha taifa au namba ya kitambulisho cha taifa;

(c) mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za mfanyakazi wa kampuni kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa
(d) mtoa huduma atatunza taarifa za mfanyakazi na kampuni;
(e) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa kwa jina la mfanyakazi; na
(f) kampuni itamtaarifu mtoa huduma kuhusu kubadili umiliki wa laini ya simu kwa ajili ya mtoa huduma kumsajili mfanyakazi mpya kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa taasisi

9. Utaratibu wa kusajili laini ya simu endapo mteja ni taasisi, utafanyika chini ya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa taasisi kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo-
(a) mwakilishi wa taasisi atawasilisha barua ya utambulisho kutoka katika taasisi husika;
(b) mwakilishi wa taasisi atawasilisha kwa mtoa huduma kitambulisho cha Taifa au Namba ya kitambulisho cha Taifa;
(c) Mtoa huduma atafanya usajili wa kundi la laini za simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za mwakilishi wa taasisi mara moja kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;
(d) mtoa huduma atatunza taarifa za taasisi na mwakilishi wa taasisi; na
(e) laini za simu zilizosajiliwa zitakuwa kwa jina la taasisi.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mtoto

10. Utaratibu wa kusajili laini za simu endapo mteja ni mtoto, utafanyika chini ya usajili wa laini za simu kibayometriki kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo:
(a) mzazi au mlezi atawasilisha nakala iliyothibitishwa ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto, nakala ya cheti cha kuasili, hati halali ya kusafiria pamoja na picha ya mtoto husika;

(b) kwa mtoto ambaye ni mzawa au mgeni, mzazi au mlezi wake atawasilisha kwa mtoa huduma kitambulisho cha taifa na mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za mzazi au mlezi kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;

(c) kwa mtoto ambaye ni mgeni wa muda mfupi, mzazi au mlezi wake atawasilisha kwa mtoa huduma hati ya kusafiria, na mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za mzazi au mlezi kupitia mfumo wa Idara ya Uhamiaji;

(d) kwa mtoto ambaye ni mdiplomasia, mzazi au mlezi wake atawasilisha hati halali ya kidiplomasia na kitambulisho cha kidiplomasia kwa ajili ya usajili wa laini ya simu;

(e) kwa mtoto ambaye ni mkimbizi, mzazi au mlezi wake atawasilisha kwa mtoa huduma kitambulisho cha ukimbizi kilichotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, na mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa ajili ya uhakiki;

(f) mtoa huduma atatunza taarifa za mtoto na mzazi au mlezi kwa njia ya kielektroniki;

(g) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa kwa jina la mtoto;

(h) baada ya kufikia umri wa utu uzima, mtoto atasajili upya laini ya simu kwa kutumia kitambulisho chake cha Taifa;

(i) mtoa huduma atamtaarifu mtoto miezi mitatu kabla ya kufikia umri wa utu uzima na atampa muda wa nyongeza wa miezi mitatu kwa ajili ya kusajili upya laini ya simu baada ya kufikia umri wa utu uzima; na

(j) endapo mtoto atashindwa kusajili upya laini ya simiu ndani ya muda wa miezi mitatu baada ya kufikia umri wa utu uzima, mtoa huduma atasitisha matumizi ya laini ya simu

husika.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mgeni wa muda mfupi

11.-(1) Utaratibu wa kusajili laini ya simu endapo mteja ni mgeni wa muda mfupi, utafanyika chini ya usajili wa laini za simu kibayometriki kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo-

(a) mgeni wa muda mfupi atawasilisha nakala ya nyaraka za kusafiria;
(b) mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za mgeni wa muda mfupi kupitia mfumo wa Idara ya Uhamiaji;
(c) mtoa huduma atatunza taarifa za mgeni wa muda mfupi;
(d) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa na jina la mgeni wa muda mfupi; na
(e) laini ya simu itakuwa hai kwa kipindi ambacho mgeni wa muda mfupi ameruhusiwa kukaa nchini.

(2) Endapo taarifa za kibayometriki au ya hati ya kusafiria hazipo katika kanzidata ya uhamihaji au kanzidata ya uhamihaji haipatikani, laini ya simu itasajiliwa kwa namna ifuatayo:

(a) mgeni wa muda mfupi ataruhusiwa kusajili laini moja tu;
(b) mteja atawasilisha hati ya kusafiria kwa ajili ya usajili wa laini ya simu;
(c) alama za vidole hazitachukuliwa wakati wa usajili wa laini ya simu;
(d) mtoa huduma atatunza nakala ya hati ya kusafiria;
(e) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa hai kwa muda ambao mgeni wa muda mfupi ameruhusiwa kukaa nchini;
(f) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa kwa jina la mgeni wa muda mfupi; na
(g) mtoa huduma atatunza taarifa za usajili na kuziwasilisha kwa Mamlaka kwa wakati.

Utaratibu wa

12. Utaratibu wa usajili wa laini za simu endapo

usajili wa laini ya simu kwa mgeni

mteja ni mgeni utafanyika chini ya usajili wa laini za simu kibayometriki kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo:

(a) mgeni atawasilisha kitambulisho alichopewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;
(b) mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;
(c) mtoa huduma atatunza taarifa za mgeni;
(d) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa kwa jina la mgeni; na
(e) laini ya simu itakuwa hai kwa kipindi ambacho mgeni ameruhusiwa kukaa nchini.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa mkimbizi

13. Utaratibu wa usajili wa laini za simu endapo mteja ni mkimbizi utafanyika chini ya usajili wa laini za simu kibayometriki kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo:

(a) mkimbizi atawasilisha kitambulisho alichopewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;
(b) mtoa huduma atafanya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za mkimbizi kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;
(c) mtoa huduma atatunza taarifa za mkimbizi na;
(d) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa kwa jina la mkimbizi.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa wanadiplomasia

14. Utaratibu wa usajili wa laini za simu endapo mteja ni mdiplomasia utafanyika chini ya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo:

(a) mdiplomasia atawasilisha hati yake halali ya kusafiria na utambulisho halali wa kidiplomasia kwa ajili ya usajili wa laini ya simu;
(b) alama za vidole hazitachukuliwa wakati wa usajili wa laini ya simu;

(c) mtoa huduma atatunza taarifa za mdiplomasia; na
(d) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa kwa jina la mdiplomasia.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa taasisi ya kidiplomasia

15. Utaratibu wa usajili wa laini za simu endapo mteja ni taasisi ya kidiplomasia utafanyika chini ya usajili wa laini ya simu kibayometriki kwenye maduka ya watoa huduma au mawakala kwa namna ifuatayo:
(a) taasisi ya kidiplomasia itawasilisha barua za utambulisho kutoka kwenye taasisi husika na Wizara yenye dhamana na masuala ya mambo ya nje;
(b) mwakilishi wa taasisi ya kidiplomasia atawasilisha hati halali ya kusafiria na kitambulisho halali cha kidiplomasia kwa ajili ya usajili wa kundi la laini za simu;
(c) alama za vidole hazitachukuliwa wakati wa usajili wa laini ya simu;
(d) mtoa huduma atatunza taarifa ya taasisi ya kidiplomasia na za mwakilishi; na
(e) laini ya simu iliyosajiliwa itakuwa kwa jina la taasisi ya kidiplomasia.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu itakayotumika kwenye kifaa cha kielektriniki au mashine

16. Utaratibu wa usajili wa laini ya simu inayotumika au inayokusudiwa kutumika kwenye mashine aukifaa kingine cha mawasiliano cha kielektroniki laini hiyo ya simu itasajiliwa kwenye maduka ya mtoa huduma kwa namna ifuatayo-
(a) endapo mashine au kifaa kingine cha mawasiliano cha kielektroniki kinamilikiwa na mtu binafsi, usajili wa laini ya simu utafanyika kibayometriki kwa mtu binafsi kama ilivyoainishwa chini ya kanuni ya 6;
(b) endapo mashine au kifaa kingine cha mawasiliano cha kielektroniki kinamilikiwa na kampuni au taasisi, usajili wa laini ya simu utafanyika kibayometriki kwa kampuni au taasisi kama ilivyoainishwa chini ya kanuni ya 7 au ya kanuni ya 9; na

(c) endapo kundi la laini za simu zitahtajika kusajiliwa kwa ajili ya kampuni au taasisi, mtoa huduma atafanya usajili wa kundi la laini za simu kibayometriki kwa kuhakiki alama za vidole za mwakilishi wa kampuni au taasisi mara moja kupitia mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa watumiaji wenye kasoro kwenye vidole au wasio na vidole

17.-(1) Utaratibu wa usajili wa laini ya simu endapo mteja ana kasoro katika alama za vidole au hana vidole utafanyika kwa namna ifuatayo:

(a) mteja atatembelea Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kuhuisha taarifa za kasoro za alama za vidole kwenye kanzidata;

(b) mteja atawasilisha kitambulisho chake cha taifa au Namba ya Utambulisho wa taifa kwa ajili ya usajili wa laini ya simu;

(c) mtoa huduma atawasilisha kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa namba ya utambulisho wa mteja kwa uhakiki wa usajili wa laini ya simu kielektroniki;

(d) baada ya kupokea maombi kwa ajili ya uhakiki, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itatoa maswali mbalimbali yasiyo na mpangilio moja kwa moja kwa mteja kwa ajili ya uhakiki wa taarifa zake kabla ya kukamilika kwa mchakato wa usajili;

(e) mtoa huduma atamuuliza maswali mteja kama alivyopokea kutoka kwenye kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;

(f) Endapo mteja atajibu angalau maswali matatu kati ya matano kwa usahihi, uhakiki utakuwa umefaulu.

(2) Mtoa huduma atatunza kumbukumbu zilizohakikiwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

(3) Endapo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itaweka utaratibu mwingine wa uhakiki kwa wateja wenye kasoro za alama za vidole, Mamlaka itatoa utaratibu mwingine wa uhakiki kama itakavyoona inafaa.

Utaratibu wa usajili wa laini ya simu kwa baadhi ya watu

18.-(1) Utaratibu wa usajili wa laini za simu endapo mteja ni mgeni wa muda mfupi na ana umri zaidi ya miaka sitini na tano, ana kasoro katika alama za vidole, hana vidole au ameingia kupitia mipaka ambayo haina vifaa vya kibayometriki utafanyika kwa namna ifuatayo:

(a) Idara ya Uhamihaji itaweka kanzidata maalumu kwa ajili ya wageni wa muda mfupi wenye umri zaidi ya miaka sitini na tano, walio na kasoro katika alama za vidole, wasiokuwa na vidole au walioingia kupitia mipaka isiyokuwa na vifaa vya usajili wa kibayometriki;

(b) aina hii ya usajili wa laini za simu utafanyika katika maduka ya watoa huduma;

(c) mteja atawasilisha hati yake ya kusafiria kwa ajili ya usajili wa laini za simu;

(d) mtoa huduma atawasilisha kwa Idara ya Uhamiaji kielektroniki namba ya hati ya kusafiria ya mteja kwa ajili ya uhakiki wakati wa usajili wa laini ya simu;

(e) baada ya kupokea maombi kwa ajili ya uhakiki, Idara ya Uhamiaji itatoa maswali mbalimbali yasiyo na mpangilio moja kwa moja kwa mteja kwa ajili ya uhakiki wa taarifa zake kabla ya kukamilika mchakato wa usajili;

(f) mtoa huduma atatumia chaguo la maswali mengi kumhakiki mteja na atauliza maswali kama alivyoyapokea kutoka kwenye kanzidata ya Idara ya Uhamihaji;

(g) endapo mteja atajibu angalau maswali matatu kati ya matano kwa usahihi, uhakiki utakuwa umefaulu.

(2) Mtoa huduma atatunza kumbukumbu zilizohakikiwa na Idara ya Uhamiaji.

(3) Endapo Idara ya Uhamiaji itaweka utaratibu mwingine wa uhakiki kwa wateja wenye kasoro za alama za vidole, Mamlaka itatoa utaratibu mwingine wa uhakiki kama itakavyoona inafaa.

Utaratibu wa

19. Endapo mteja ambaye jina lake limesajiliwa

kusajili upya laini ya simu

na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, amebadili jina, mteja huyu atatuma taarifa za mabadiliko hayo kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa na utaratibu wa kusajili upya laini ya simu utakuwa kama ulivyoainishwa chini ya kanuni ya 6,7 au 9.

Zuio la kutumia kitambulisho cha taifa

20. Mgeni, mgeni wa muda mfupi, mkimbizi au mdiplomasia hatatumia kitambulisho cha taifa kilichotolewa kwa raia wa Tanzania kwa lengo la usajili wa laini ya simu.

Haki ya kusajili laini ya simu bila uthibitisho wa kibiometriki

21. Mteja kutoka taasisi ya Serikali au wakala aliyeidhinishwa na Serikali ambaye anahitaji msamaha wa usajili wa laini ya simu kwa njia ya kibayometriki atatumia utaratibu ufuatao:

(a) ataandika barua kwa Mamlaka ili kupata kibali cha msamaha wa usajili wa laini ya simu kwa njia ya kibayometriki;
(b) atawasilisha kitambulisho chake cha taifa au Namba ya kitambulisho cha taifa na kibali cha Mamlaka kwa mtoa huduma kwa ajili ya usajili wa laini ya simu;
(c) mtoa huduma atasajili laini ya simu kwa idhini ya Mamlaka; na
(d) usajili wa laini ya simu ya aina hii utafanywa katika maduka ya watoa huduma.

Taarifa ya ziada

22. Mtu yeyote anayeuza, kusajili au kwa namna nyingine yoyote anatoa laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu anaweza kuomba taarifa ya ziada kutoka kwa mteja inayohusiana na usajili wa laini ya simu.

## SEHEMU YA TATU
## KUHUISHA NA KUSITISHA MATUMIZI YA LAINI ZA SIMU

Kuhuisha matumizi ya laini za simu

23.-(1) Mtoa huduma hatahuisha matumizi ya laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano

kinachotumia laini ya simu kwenye mfumo wake wa mawasiliano ya kielektroniki isipokuwa kama usajili wa laini ya simu umefanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Taarifa za usajili wa laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu zitawekwa kwenye kanzidata ya mtoa huduma baada ya kuhakikiwa kupitia kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa au Idara ya Uhamiaji na itawasilishwa kwa wakati kwenye kanzidata Kuu ya Usajili wa Laini za simu.

(3) Usajili wa laini ya simu yoyote inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu ambao haujahakikiwa kupitia kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Idara ya Uhamiaji au kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi, utakuwa batili.

(4) Laini ya simu iliyosajiliwa kwa ajili ya mgeni wa muda mfupi itakuwa hai kwa muda ambao mgeni ameidhinishwa kukaa nchini.

(5) Mtoa huduma atahakikisha kuwa-

(a) laini yoyote ya simu ambayo ni mpya, inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu inakuwa na PIN;

(b) PIN ya laini ya simu imezimwa wakati wa usajili wa laini ya simu;

(c) wateja wamewekewa chaguo la kuwasha au kuzima PIN kwa ajili ya usalama wa laini ya simu;

(d) elimu na ushauri kuhusu umuhimu na namna ya kutumia PIN kwenye laini ya simu inatolewa kwa wateja.

Uhuishaji wa matumizi ya PIN ya kufungua na kufunga laini ya simu

24.-(1) Uhuishaji wa matumizi ya PIN ya laini ya simu kwenye simu za mkononi utakuwa kwa namna ifuatayo-

(a) mtoa huduma atamfahamisha mteja wakati wa usajili wa laini ya simu kwamba laini za simu zimewezeshwa PIN na kumshauri mteja

kutumia PIN kwa usalama wake binafsi;

(b) baada ya kuweka laini ya simu kwenye simu ya mkononi, ujumbe mfupi utapokelewa moja kwa moja na taarifa kuhusu utaratibu wa kuwezesha, kubadilisha na kuzima PIN; na

(c) endapo PIN ya laini ya simu imehuishwa, itatakiwa kufanya kazi wakati wote simu itakapowashwa au kuzimwa.

(2) Uwezeshaji wa PIN kwenye laini za simu zinazotumiwa kwa mawasiliano ya mashine kwa mashine na vifaa vingine vinavyohusiana itakuwa kwa namna ifuatayo:

(a) wakati wa usajili wa laini ya simu, mteja atatoa namba ya simu mbadala au atapewa kiungo kwa ajili ya laini za simu zote zinazotumika kwa mawasiliano ya mashine kwa mashine na vifaa vingine vinavyohusiana ili kupata taarifa ya PIN;

(b) baada ya kuweka laini ya simu kwenye kifaa, ujumbe mfupi utapokelewa moja kwa moja kwenye namba ya simu mbadala au kiungo na taarifa kuhusu utaratibu wa kuwezesha, kubadilisha na kuzima PIN.

(3) Endapo mteja ataweka PIN kwenye laini ya simu kwa kukosea mara tano mfululizo, laini ya simu itasitishwa matumizi na mteja atatakiwa kumuomba mtoa huduma kuhuisha laini ya simu husika.

Uzimaji wa laini za simu zisizotumika

25.-(1) Endapo laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu haijatumika katika mawasiliano kwa muda wa siku tisini mfululizo, laini hiyo ya simu itasitishwa kutumika.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtoa huduma hatasitisha matumizi ya laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu pale ambapo mteja ametoa taarifa kwa maandishi kuwa laini hiyo ya simu haitatumika kwa kipindi cha mfululizo cha miezi isiyozidi kumi na miwili.

(3) Mteja ambaye laini yake ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu kimesitishwa matumizi anaweza kuwasilisha maombi mapya ya usajili ili kupata namba yake ya awali ikiwa bado ipo.

(4) Endapo mteja atafariki, ndani ya siku tisini baada ya kifo-

(a) mume, mke, watoto au ndugu wa karibu atatoa taarifa ya kifo hicho kwa mtoa huduma husika;

(b) msimamizi wa mirathi ndani ya kipindi cha miezi sita atawasilisha taarifa za mtu atakayerithi laini ya simu na mtoa huduma hatasitisha matumizi ya laini hiyo na mrithi huyo atatakiwa kufuata taratibu zote za usajili wa laini ya simu;

(c) endapo hakuna mrithi wa laini ya simu, msimamizi wa mirathi atarudisha laini hiyo ya simu kwa mtoa huduma husika kabla ya kuisha kwa kipindi cha miezi sita.

Utaratibu kwa ajili ya mizani au bakaa ya fedha Sura ya 437

26. Mtoa huduma ataweka utaratibu wa kushughulikia salio la fedha lililopo katika laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu ambacho kimehuishwa matumizi yake kwa mujibu wa Sheria ya Mfumo wa Malipo wa Taifa.

Uwasilishaji wa maelezo ya uzimaji wa laini za simu kwa Mamlaka

27. Mtoa huduma atawasilisha kwa Mamlaka taarifa za laini za simu zinazoweza kuondolewa, zilizojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano cha simu kinachotumia laini za simu ambazo zimesitishwa matumizi yake kwa wakati na katika muundo utakaoamuliwa na Mamlaka.

## SEHEMU YA NNE
## UTUMIAJI WA MAWAKALA KATIKA USAJILI WA LAINI ZA SIMU

Utumiaji wa mawakala kwenye usajili wa laini za simu

28.-(1) Mtoa huduma anaweza kutumia mawakala walioidhinishwa katika kusajili laini za simu zinazoweza kuondolewa, zilizojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu.

(2) Wakala anayesajili laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano cha simu kinachotumia laini ya simu atakuwa na mkataba halali na kadi za utambulisho halali zinazotolewa na mtoa huduma katika mfumo ulioidhinishwa na Mamlaka.

(3) Wakala anaweza kufanya kazi katika eneo mahususi au eneo lenye mipaka ya kijiografia.

(4) Mtoa huduma hataruhusu wakala asiye na mkataba halali kutumia mfumo wa usajili wa mtoa huduma.

Uhitaji wa mawakala

29.-(1) Kila mtoa huduma atahakikisha kwamba kila wakala aliyetajwa chini ya kanuni ya 28(1) ambaye ameidhinishwa kupata laini ya simu iliyosajiliwa katika mfumo atapaswa kutimiza masharti yafuatayo:

(a) ikiwa ni mawakala ambao wanatoa huduma katika maduka watatakiwa kuwa na -
   (i) leseni ya biashara;
   (ii) namba ya utambulisho ya mlipa kodi;
   (iii) anuani ya biashara ambayo inajumuisha jina la mtaa, namba ya nyumba na postikodi;
   (iv) Jina la mhusika na anuani yake;
   (v) mawasiliano ikijumuisha namba ya simu na barua pepe;
   (vi) mkataba halali wa mtoa huduma; na
   (vii) kitambulisho halali cha Taifa cha mhusika;
(b) ikiwa ni wakala wa simu ambaye hana ofisi maalumu-
   (i) anuani ya makazi ambayo inajumuisha jina la muhusika, mtaa, namba ya nyumba na postikodi;
   (ii) mawasiliano ikijumuisha namba ya simu na barua pepe;

(iii) hati safi ya polisi inayohuishwa kila mwaka;
(iv) mkataba halali na mtoa huduma;
(v) kitambulisho halali cha taifa;
(vi) namba ya utambulisho wa mlipa kodi;
(vii) kitambulisho halali kilichotolewa na mtoa huduma.

Uwasilishaji wa taarifaza mwezi na mtoa huduma

30. kila mtoa huduma atawasilisha kila mwezi ripoti inayohakiki orodha ya mawakala wote walioidhinishwa na Mamlaka.

## SEHEMU YA TANO
## UBADILISHAJI WA TAARIFA AU UMILIKI

Ubadilishaji wa taarifa na umiliki

31.-(1) Maombi ya kubadilisha umiliki wa laini ya simu yatawasilishwa kwenye duka la mtoa huduma ambapo mtoa huduma atatafuta ridhaa ya mabadiliko hayo kutoka kwa mmiliki wa awali.

(2) Mmiliki wa awali anaweza kuridhia au kukataa maombi ya kubadilisha umiliki wa laini ya simu yaliyowasilishwa kwa mtoa huduma.

(3) Endapo mmiliki wa awali ataridhia, mtoa huduma atasajili laini ya simu kwa njia ya kibayometriki na kuhifadhi taarifa za mmiliki wa awali na mmiliki mpya.

Jukumu la kutoa taarifa ya kupotea kwa laini ya simu

32. Mteja wa laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu atalazimika:

(a) kutoa taarifa ya kupotea au kuibiwa kwa laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu katika kituo cha polisi na kupata taarifa ya kupotea kwa laini ya simu husika au ripoti ya uchunguzi wa awali ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kupotea au kuibiwa kwa laini hiyo ya simu;

(b) kuwasilisha kitambulisho cha Taifa, namba ya utambulisho cha Taifa au hati ya kusafiria kwa mtoa huduma wake wakati atakapohitaji kubadilisha laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu.

Ubadilishaji wa laini ya simu

33.-(1) Mtoa huduma atabadilisha laini ya simu iliyopotea, iliyoibiwa au iliyoharibika baada ya uhakiki wa umiliki wake.

(2) Mteja atakabidhi laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu ambayo imeharibika, kabla ya kuibadilisha.

(3) Mtoa huduma atahakikisha kuwa laini ya simu iliyotajwa katika kanuni ndogo ya (2) inatunzwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili.

Kubadili taarifa kwenye simu

34.-(1) Mtoa huduma atahakikisha kuwa laini za simu zote zilizobadilishwa zimehakikiwa kibayometriki au zimehakikiwa kwa namna ilivyowekwa chini ya kanuni hizi.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), mtoa huduma-

(a) atawasilisha kwa Mamlaka taratibu zake za kubadili laini ya simu;

(b) atahifadhi taarifa za usajili wa laini ya simu zilizobadilishwa;

(c) atatunza laini ya simu inayoweza kuondolewa, iliyojengwa ndani ya simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano kinachotumia laini ya simu iliyoharibika;

(d) atarekodi na kuhifadhi taarifa za wakala aliyehamisha taarifa za laini ya simu pamoja na za mtu yeyote mwenye uwezo wa kuingia na kutumia kanzidata inayotunza uhamishaji wa taarifa kwenye laini mpya;

(e) atatunza taarifa zote alizozipata chini ya kanuni hii kwenye kanzidata itakayofikika kwa urahisi kwa kipindi cha miezi kumi na

miwili.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Uhitaji wa wakala kukaguliwa

35. Mtoa huduma atamkagua wakala wake kila mwezi kuhakikikisha kuwa matakwa ya usajili wa laini za simu yanazingatiwa na kuwasilisha taarifa ya mwezi kwa Mamlaka.

Kuzuia udanganyifu

36. Watoa huduma wote watadhibiti vitendo vya udanganyifu wakati wa usajili wa laini za simu kwa kuzingatia yafuatayo:

(a) kutekeleza taratibu za ndani za kudhibiti vitendo vya udanganyifu wakati wa usajili wa laini za simu;
(b) kusitisha matumizi ya laini zote za simu ambazo zimebainika kuwa zimesajiliwa kwa udanganyifu;
(c) kushirikiana pale inapowezekana, kuzuia vitendo vya udanganyifu au vitendo ambavyo havijaidhinishwa wakati wa usajili wa laini za simu na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika wa vitendo vya udanganyifu;
(d) kuhakikisha ulinzi na usiri wa taarifa kwa kufuata sheria husika zinazotumika pamoja na sheria nyingine za makampuni na biashara;
(e) kufidia waathirika wa upotevu wowote wa pesa na mali utakaotokana na vitendo vya udanganyifu unaohusiana na usajili wa laini za simu ambapo mtoa huduma alishindwa kumtambua mhusika aliyefanya udanganyifu;
(f) kuweka zuio la kuendelea kutumika katika usajili wa laini za simu, namba za kitambulisho cha taifa au hati ya kusafiria iliyotumika kusajili laini ya simu ambayo imebainika katika kitendo cha udanganyifu;
(g) kuweka zuio la kuendelea kutumika kwa namba tambulishi za vifaa vyote vya kielektroni na mawasiliano ambavyo

vimebainika kutumika katika vitendo vya udanganyifu;

(h) kuwasilisha kwa Mamlaka, taarifa zote za namba ya kitambulisho cha taifa au hati ya kusafiria, namba ya laini ya simu na namba tambulishi ya kifaa ambazo zimefungiwa kwa ajili ya kuwataarifu watoa huduma wengine ili waweze kuzizuia kutumika katika mitandao yao; na

(i) kuwaondoa kwenye mfumo wa usajili wa laini za simu mawakala wote waliobainika kuhusika kwenye vitendo vya udanganyifu wakati wa usajili wa laini za simu;

(j) kuwasilisha taarifa za mawakala walioondolewa kwenye mifumo ya usajili wa laini za simu kwa Mamlaka ya kuwasilishwa kwa watoa huduma wengine kwa hatua stahiki; na

(k) kutekeleza utaratibu mwingine wowote kama utakavyoidhinishwa na Mamlaka.

Ukomo wa umiliki wa idadi za laini za simu

37.-(1) Mtu anayekusudia kumiliki na kutumia laini ya simu inayoweza kutolewa, laini ya simu iliyojengewa ndani au kifaa cha mawasiliano kilichowezeshwa na laini ya simu ataruhusiwa kusajili-

(a) ikiwa ni mtu binafsi-

(i) laini ya simu moja pekee kwa kila mtandao wa simu kwa ajili ya matumizi ya sauti, ujumbe mfupi na huduma za kimtandao;

(ii) laini za simu zisizozidi tano kwa kila mtandao wa simu kwa ajili ya matumizi ya mawasiliano ya mashine kwa mashine; na

(b) ikiwa ni kampuni au taasisi, atasajili-

(i) laini za simu zisizozidi mia moja kwa kila mtandao wa simu kwa ajili ya matumizi ya sauti, ujumbe mfupi na huduma za mtandao; na

(ii) laini za simu zisizozidi mia mbili

kutoka kwa kila mtandao wa simu kwa ajili ya matumizi ya mawasiliano ya mashine kwa mashine.

(2) Laini ya simu iliyosajiliwa chini ya kanuni ndogo ya (1) haitatumika kwa matumizi tofauti na yaliyokusudiwa wakati wa usajili.

(3) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), mtu binafsi, kampuni au taasisi inaweza kuruhusiwa kusajili au kumiliki zaidi ya idadi ya laini za simu zilizoainishwa baada ya kupokea ridhaa ya kusajili laini ya ziada kutoka kwa Mamlaka.

(4) Mamlaka inaweza kuweka ukomo wa laini za ziada kwa aina ya usajili.

(5) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), mtu binafsi, kampuni au taasisi itawasilisha sababu za msingi kwa kila ombi la laini za simu za ziada.

(6) Mtu ambaye atakiuka kanuni hii, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kama ifuatavyo-

(a) endapo ni mtu binafsi, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi kumi na miwili au vyote na atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu sabini na tano kwa kila siku ambayo laini ya simu husika ilitumika au kumilikiwa; na

(b) ikiwa ni kampuni au taasisi, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini na atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu sabini na tano kwa kila siku ambayo laini ya simu husika ilitumika au kumilikiwa.

Uthibitishaji wa laini za simu zilizopo

38.-(1) Endapo mtu binafsi au kampuni au taasisi inamiliki idadi ya laini za simu zaidi ya zilizoainishwa katika kanuni ya 37(1), mtoa huduma atamtaarifu mteja husika ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa kanuni hizi ili achague namba kuu ya laini ya simu na kuhakiki namba za ziada pasipo kuzidisha kikomo cha idadi kilichoainishwa katika

Kanuni hizi.

(2) Baada ya kushindwa kuzingatia matakwa yaliyowekwa chini ya kanuni ndogo ya (1), mtoa huduma atasitisha matumizi ya laini zote za simu ambazo hazijahakikiwa ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kutolewa kwa notisi.

(3) Endapo mtoa huduma atashindwa, ataacha au atazembea kuzingatia matakwa chini ya kanuni ndogo ya (1) na ya (2), atalipa faini isiyopungua shilingi milioni tano.

(4) Endapo laini ya simu iliyosajiliwa imesitishwa matumizi chini ya kanuni ndogo ya (2) na mmiliki ana nia ya kuihuisha, mtoa huduma anaweza kuisajili upya laini hiyo ya simu kwa kuzingatia upatikanaji wake.

Kosa kwa utumiaji mbaya wa taarifa

39. Mtoa huduma au wakala yeyote atakayetumia taarifa ya mteja vibaya kwa ajili ya usajili wa laini ya simu, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo cha kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili au vyote.

Adhabu ya jumla

40.-(1) Mtu yeyote atakayekiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi pale ambapo hakuna adhabu mahususi iliyowekwa, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa chini ya Sheria.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), endapo mtu atakuwa ametenda kosa chini ya Kanuni hizi, Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka anaweza, pale ambapo mtu huyo amekubali kwa maandishi, kufifilisha kosa hilo kwa namna ilivyoainishwa kwenye Sheria.

Kufutwa kwa TS Na. 112 la 2020

41. Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Usajili wa laini za Simu za Mwaka 2020 zimefutwa.

Dodoma,
1 Februari, 2023

NAPE MOSES NNAUYE,
*Waziri wa Habari, Mawasiliano*
*Na Teknolojia ya Habari*